**SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA BARAZA LA WAWAKILISHI (KINGA, UWEZO NA FURSA), NAM. 4 YA 2007 NA KUTUNGA SHERIA MPYA YA BARAZA LA WAWAKILISHI (KINGA, UWEZO NA FURSA) KATIKA KUTEKELEZA KAZI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**


**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Ufafanuzi.

**SEHEMU YA PILI**
**FURSA NA KINGA ZA WAJUMBE NA MAAFISA WA BARAZA**

3. Uhuru wa kujieleza na mjadala.
4. Kinga dhidi ya hatua za kisheria.
5. Uhuru wa kutokukamatwa kutokana na madai ya madeni.
6. Wito kutokutekelezwa ndani ya eneo la Baraza.
7. Uhuru wa Mjumbe kufanya mkutano katika Jimbo lake.
8. Bendera ya Baraza na matumizi yake.
9. Mjumbe kupatiwa taarifa.
10. Utaratibu wa kuingia katika eneo la Baraza.
11. Uwezo wa Spika kutoa amri ya kuondoka katika eneo la Baraza.
12. Mamlaka na utaratibu kuhusiana na uvunjwaji wa haki za Baraza.
13. Kanuni za Maadili za Wajumbe.

## SEHEMU YA TATU
## USHAHIDI

14. Uwezo wa kuita mashahidi.

15. Kutoa taarifa ya wito.

16. Uwezo wa kutoa Hati ya kumlazimisha shahidi kuhudhuria.

17. Shahidi anaweza kuhojiwa kwa kiapo.

18. Kukataa kujibu suali au kutoa nyaraka.

19. Fursa za shahidi.

20. Ushahidi wa Mwenendo wa Mashauri katika Baraza au Kamati kutokutolewa bila ya ruhusa.

21. Cheti kwa Shahidi.

22. Ushahidi wa uongo.

23. Kuingilia ushahidi.

24. Waraka wa uongo.

25. Kudharau.

26. Maswali yanayohusiana na maamuzi ya ushahidi na utoaji wa nyaraka.

27. Taratibu za Baraza kuwa za kimahakama.

## SEHEMU YA NNE
## MAKOSA NA ADHABU

28. Kosa kuhusu uingiaji katika Baraza.

29. Rushwa au utendaji mbaya.

30. Makosa mengine dhidi ya Mjumbe na Afisa wa Baraza.

31. Kukosa utiifu.

32. Makosa mengine.

33. Kupokea rushwa kwa Mjumbe.

34. Kulindwa kwa mtu anayechapisha kwa mamlaka ya Baraza.

35. Kutangaza mwenendo wa kesi bila ya nia ovu.

36. Mtu asiyekuwa na sifa kukaa au kupiga kura ndani ya Baraza.

**SEHEMU YA TANO**
**MASHARTI YA JUMLA**

37. Kutokamatwa bila ya idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

38. Taarifa juu ya kukamatwa kwa Mjumbe.

39. Kinga.

40. Uwezo wa Mpambe wa Baraza.

41. Uwezo wa kukamata.

42. Idhini kwa ajili ya mashtaka.

43. Taarifa Rasmi iliyochapishwa kutokana na amri ya Baraza kukubaliwa kwa ajili ya ushahidi.

44. Hadhi ya uwezo chini ya Sheria hii.

45. Kutokuwepo kwa Spika au Naibu Spika.

46. Tuhuma juu ya afya ya akili ya Mjumbe.

47. Katibu kuandaa toleo juu ya Haki na Fursa za Mjumbe.

48. Wajibu wa Mjumbe.

49. Yasiyohusika kwa Wajumbe na Maafisa wa Baraza.

50. Adhabu kwa Mjumbe.

51. Adhabu ya jumla.

52. Kutotekelezwa kwa Hukumu.

53. Kanuni.

54. Kufuta na kubakiza.

**Jadweli**

**SHERIA NAM. 6 YA 2022**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

**6/10/, 2022**

# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA BARAZA LA WAWAKILISHI (KINGA, UWEZO NA FURSA), NAM. 4 YA 2007 NA KUTUNGA SHERIA MPYA YA BARAZA LA WAWAKILISHI (KINGA, UWEZO NA FURSA) KATIKA KUTEKELEZA KAZI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Baraza la Wawakilishi (Kinga, Uwezo na Fursa), 2022 na itasomwa pamoja na Sura ya Tano ya Katiba na itaanza kutumika mara tu baada ya kutiwa saini na Rais.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo:

"Msaidizi wa Mjumbe" maana yake ni mtu ambaye anamsaidia Mjumbe mwenye mahitaji maalum katika utekelezaji wa shughuli za Baraza au Kamati;

"Kamati" maana yake ni Kamati ya Kudumu ya Baraza na inajumuisha Kamati Teule na Kamati nyengine zozote zitakazoanzishwa kwa mujibu wa Katiba na masharti ya Kanuni za Kudumu kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Baraza;

"Katiba" maana yake ni Katiba ya Zanzibar ya 1984;

"Mwenyekiti wa Kamati" maana yake ni Mjumbe yeyote aliyechaguliwa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu kuongoza Kamati yoyote na inajumuisha Makamu Mwenyekiti na Mjumbe mwengine yeyote atakayechaguliwa na Kamati kuongoza kikao pale ambapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo;

"Katibu" maana yake ni Katibu wa Baraza na inajumuisha Msaidizi wa Katibu au Mtumishi mwengine yeyote wa Baraza aliyeidhinishwa kutekeleza kazi yoyote ya Katibu;

"Mkurugenzi wa Mashtaka" maana yake ni mtu aliyeteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka chini ya masharti ya Katiba;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Baraza" maana yake ni Baraza la Wawakilishi la Zanzibar lililoanzishwa kwa mujibu wa Katiba na linajumuisha Kamati ya Baraza zima au Kamati nyengine yoyote ya Baraza;

"Taarifa Rasmi" maana yake ni kumbukumbu za mwenendo wa Baraza au majadiliano ya Baraza au kumbukumbu rasmi ya upigaji kura ndani ya Baraza ambayo imetayarishwa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu;

"Mjumbe" maana yake ni Mjumbe wa Baraza na inajumuisha Spika ikiwa Spika sio Mjumbe wa Baraza;

"Mkutano" maana yake ni mfululizo wa vikao vya Baraza kuanzia kikao cha kwanza hadi kufikia wakati ambapo shughuli zote zilizopangwa kwa ajili ya mkutano huo zitakuwa zimekamilika;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana na mambo yanayohusiana na Baraza;

"Afisi ya Baraza" maana yake ni Afisi ya Baraza iliyoanzishwa na kufanya kazi zake kwa mujibu wa Katiba na sheria zinazohusika;

"Afisa wa Baraza" maana yake ni Katibu au Afisa mwengine yeyote au mtu anayefanya kazi katika eneo la Baraza chini ya amri ya Spika na inajumuisha Afisa wa Polisi yeyote aliopo kazini ndani ya eneo la Baraza;

"Afisa wa Polisi" maana yake ni Mjumbe yeyote wa Jeshi la Polisi kama ilivyotafsiriwa na Sheria inayohusiana na Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi, Sura ya 322;

"Eneo la Baraza" maana yake ni ukumbi ambao Baraza linakutana kutekeleza shughuli zake pamoja na ofisi, vyumba, kumbi kwa ajili ya shughuli mbali mbali, bustani na eneo jengine lolote linalotumika kwa matumizi ya kawaida au makaazi rasmi ya Spika, majengo yaliyokuwa yakitumiwa na Baraza na njia yoyote inayounganisha na maeneo hayo na maeneo mengine yoyote yanayounganisha kama yatakavyoelezwa kila baada ya muda na Spika na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali kuwa yamo katika eneo la Baraza;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Afisa wa Umma" maana yake ni mtu yeyote aliyeajiriwa au mwenye dhamana katika ofisi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au katika Taasisi yake yoyote ya Umma ama inayojitegemea au ya huduma au afisi isiyo ya kudumu au ya muda au ya malipo au isiyo ya malipo;

"Sekretarieti" maana yake ni Kamati Tendaji ya Baraza inayomsaidia Katibu katika kutekeleza kazi zake na inajumuisha Wakuu wa Idara na Divisheni katika Muundo wa Baraza na Makatibu Kamati;

"Mpambe wa Baraza" maana yake ni Mtumishi wa Baraza anayeteuliwa na Katibu kwa ajili ya kusimamia itifaki na kudumisha usalama wa Baraza kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu;

"Kamati Teule" maana yake ni Kamati inayoundwa na Baraza kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu kwa ajili ya jambo makhsus;

"Kanuni za Kudumu" maana yake ni Kanuni za Kudumu za Baraza zilizotungwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba;

"Spika" maana yake ni Spika wa Baraza na inajumuisha Mjumbe mwengine yeyote aliyechaguliwa kuongoza kikao cha Baraza;

"Mgeni" maana yake ni mtu yeyote ambaye si Rais, Spika, Mjumbe, Katibu, Afisa wa Baraza, Afisa mwengine yeyote au mtu ambaye anatekeleza kazi maalum zinazohusu Baraza kwa kiasi tu kinachomuwezesha kufanya kazi hizo;

"Makamu Mwenyekiti" maana yake ni Mjumbe yeyote aliyechaguliwa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu.

## SEHEMU YA PILI
## FURSA NA KINGA ZA WAJUMBE NA MAAFISA WA BARAZA

Uhuru wa kujieleza na mjadala.

**3.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Kudumu, kutakuwa na uhuru wa kujieleza na mjadala katika Baraza.

(2) Uhuru wa kujieleza na mjadala kama ulivyotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hautahojiwa katika Mahkama au pahala pengine popote nje ya Baraza.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu hiki, mtu yeyote aliyepata athari mbaya kutokana na kauli au maneno ya Mjumbe yeyote anaweza kupeleka malalamiko yake kwa Spika kwa mujibu wa masharti ya Kanuni za Kudumu.

Kinga dhidi ya hatua za kisheria.

**4.** Mashauri ya madai au jinai hayatofunguliwa dhidi ya Mjumbe yeyote na Mjumbe hatowajibika kuhojiwa katika Mahkama au pahala pengine popote nje ya Baraza kwa maneno aliyoyasema au kitendo alichokifanya kwa nia njema kulingana na maamuzi ya Baraza au taarifa iliyoandikwa na Baraza au Kamati au kwa sababu ya jambo lolote au kitu kilichowasilishwa na Mjumbe huyo kwa njia ya maombi, mswada, maazimio, hoja au vyenginevyo au kwa kura aliyopiga Mjumbe huyo katika Baraza au Kamati yoyote inayohusika.

Uhuru wa kutokukamatwa kutokana na madai ya madeni.

**5.** Mjumbe hatokamatwa wakati anakwenda, anahudhuria au anarudi kutoka katika kikao cha Baraza au Kamati yoyote kwa deni lolote la kesi ya madai isipokuwa kwa deni ambalo makubaliano yake yanahusisha kosa la jinai.

Wito kutokutekelezwa ndani ya eneo la Baraza.

**6.**-(1) Bila ya kujali kitu chochote kinachopingana, hakuna wito utakaotolewa na Mahakama au mamlaka yoyote iliyopo Zanzibar au nje ya Zanzibar inayotekeleza mamlaka ya madai au jinai utakaotolewa au kutekelezwa ndani ya eneo la Baraza au kupitia kwa Spika au Afisa yeyote wa Baraza, wakati kikao kinaendelea.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mjumbe yeyote hatokamatwa kwa makosa ya madai wakati Mjumbe yumo ndani ya eneo la Baraza na wakati wa kikao cha Baraza au Kamati kinaendelea isipokuwa kwa ruhusa ya maandishi ya Spika.

Uhuru wa Mjumbe kufanya mkutano katika Jimbo lake.

**7.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii au masharti ya sheria nyengine yanayosimamia kufanyika na kutekelezeka kwa mkutano wa hadhara, Mjumbe atakuwa huru kufanya mikutano ya hadhara katika Jimbo lake na mamlaka zote husika zitamuwezesha Mjumbe katika hali iliyokuwa nzuri kwa Mjumbe kama mazingira yanavyoruhusu.

(2) Mtu ambaye anayezuia kufanyika kwa mkutano huo wa hadhara ulioelezwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa na atashitakiwa kwa mujibu wa sheria.

Bendera ya Baraza na matumizi yake.

**8.**-(1) Kutakuwa na Bendera ya Baraza ambayo itakuwa kama itakavyoainishwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Kudumu na sheria nyengine yoyote inayosimamia matumizi, kupepea au kupandishwa kwa Bendera ya Zanzibar, Mjumbe anaweza kutumia Bendera ya Baraza wakati yupo:

(a) katika Ofisi ndani ya Jimbo lake la uchaguzi;

(b) katika mkutano wa hadhara usiokuwa mkutano ulioitishwa ama na chama cha siasa au kwa madhumuni ya kampeni za uchaguzi; au

(c) safarini ndani ya Zanzibar.

(3) Waziri kwa kushauriana na Spika anaweza kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa malengo na masharti ya kifungu hiki kuhusiana na matumizi ya Bendera ya Baraza.

Mjumbe kupatiwa taarifa.

**9.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii na sheria nyengine yoyote inayohusiana na Usalama wa Taifa, Mjumbe atapatiwa taarifa yoyote anayoiomba kwa njia ya maandishi, ndani ya siku saba kwa Afisa wa Umma mwenye mamlaka ya kutoa taarifa hiyo.

(2) Taarifa zinazohusika na kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, zitaombwa kwa maandishi kupitia kwa Katibu.

(3) Iwapo Afisa wa Umma anaona kwamba taarifa iliyoombwa itachukua muda zaidi kuliko muda uliotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, anaweza kuomba kwa Katibu kuongezwa muda wa kutoa taarifa hiyo na kuongezwa huko hakutozidi siku saba.

(4) Iwapo Afisa wa Umma atashindwa kutoa taarifa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Katibu atamtaarifu Mnadhimu wa Serikali asimamie upatikanaji wa taarifa hizo ndani ya muda unaofaa.

(5) Taarifa zilizopokelewa na Mjumbe chini ya masharti ya kifungu hiki, zitatumika tu katika kutekeleza majukumu yake ya Baraza.

(6) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, Mnadhimu wa Serikali maana yake ni Kiongozi aliyeteuliwa na Serikali kutoka miongoni mwa Mawaziri kwa ajili ya kumsaidia Kiongozi wa Shughuli za Serikali kuratibu shughuli za Serikali ndani ya Baraza.

Utaratibu wa kuingia katika eneo la Baraza.

**10.**-(1) Kwa ruhusa ya Spika au Mwenyekiti wa Kamati kwa namna itakavyokuwa, Msaidizi wa Mjumbe anaweza kuingia katika eneo la Baraza ikijumuisha ukumbi wa Baraza au wa Kamati itakapotokezea haja ya kufanya hivyo.

(2) Katibu kwa maelekezo ya Spika, ataandaa utaratibu wa kuwawezesha wageni kuingia ndani ya Baraza ikijumuisha kuhudhuria katika vikao vya Baraza na Kamati zake.

Uwezo wa Spika kutoa amri ya kuondoka katika eneo la Baraza.

**11.** Spika au Afisa mwengine yeyote aliyeidhinishwa na Spika anaweza, itakapotokea haja ya kufanya hivyo katika muda wowote kumuamuru mgeni yeyote kutoka katika eneo la Baraza.

Mamlaka na utaratibu kuhusiana na uvunjwaji wa haki za Baraza.

**12.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Katiba na Kanuni za Kudumu, Baraza litakuwa na uwezo na mamlaka yote kama itakavyohitajika kwa ajili ya kuchunguza, kuamua na kutamka juu ya kufanyika kwa kitendo, jambo au kitu chochote, kisichokuwa kosa chini ya Sheria hii, kuwa ni uvunjifu wa haki za Baraza.

(2) Kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu, Spika atakuwa na uwezo wa kuamua kama kitendo chochote, jambo au kitu ambacho Baraza linaweza kuhoji, kuamua na kutamka kuwa ni uvunjifu wa haki za Baraza.

(3) Baraza au Kamati, kama itakavyokuwa, kuhusiana na kitendo chochote, jambo au kitu, linaweza kupendekeza kwa Spika kwamba amuombe Mkurugenzi wa Mashtaka kuchukua hatua zinazofaa ikiwa ataona ni haki kumshitaki mtu yeyote anayehusika katika kutenda kosa lolote chini ya Sheria hii.

(4) Spika ama kwa maamuzi yake mwenyewe au mapendekezo ya Kamati, atamuarifu Mkurugenzi wa Mashtaka juu ya vitendo, jambo au vitu vyote vilivyofanywa na mtu yeyote kuwa ni kosa chini ya Sheria hii, na Mkurugenzi wa Mashtaka ataifanyia kazi taarifa hiyo kwa mujibu wa sheria.

| | |
|---|---|
| Kanuni za Maadili za Wajumbe. | **13.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Zanzibar au sheria nyengine yoyote inayohusika, Baraza linaweza kwa kupitia Azimio kuridhia Kanuni za Maadili kwa Wajumbe wa Baraza. |

## SEHEMU YA TATU
## USHAHIDI

| | |
|---|---|
| Uwezo wa kuita mashahidi. | **14.**-(1) Baraza, Kamati au Kamati Teule inaweza, kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki na kifungu cha 20 cha Sheria hii, kumwita mtu yeyote kuhudhuria mbele ya Baraza au Kamati hiyo, kutoa ushahidi au kuwasilisha nyaraka yoyote anayoimiliki au iliyo chini ya udhibiti wa mtu huyo. |
| | (2) Uwezo uliotolewa na kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki kwa Kamati Teule, unaweza kutumiwa na Kamati nyengine yoyote ambayo imeidhinishiwa kwa azimio la Baraza kutekeleza mamlaka hayo juu ya jambo lolote au suali lililotolewa katika azimio hilo. |
| Kutoa taarifa ya wito. | **15.**-(1) Amri yoyote ya kuhudhuria, kutoa ushahidi au kutoa nyaraka mbele ya Baraza au Kamati itawasilishwa kwa mtu anayetakiwa kuhudhuria au kuwasilisha nyaraka kwa njia ya wito uliosainiwa na kutolewa na Katibu chini ya maelekezo ya Spika. |
| | (2) Katika kila wito uliotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utaeleza wakati na mahali ambapo mtu aliyeitwa anahitajika kuhudhuria na nyaraka maalum zinazohitajika kuwasilishwa na wito huo atapewa mtu aliyetajwa ndani ya wito huo ama kwa kumuwasilishia nakala ya nyaraka hiyo au kwa kuacha nakala kwa mtu mzima katika makaazi yake ya kawaida au makaazi yanayojulikana ndani ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na shahidi huyo atalipwa gharama zake kama itakavyoelezwa katika Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii. |
| | (3) Wito uliotolewa chini ya kifungu hiki unaweza kuwasilishwa na Afisa wa Baraza au Afisa wa Polisi. |
| | (4) Wito uliotolewa chini ya masharti ya kifungu hiki, utakuwa kama ulivyoelezwa katika Jadweli la Pili la Sheria hii. |
| Uwezo wa kutoa Hati ya kumlazimisha shahidi kuhudhuria. | **16.**-(1) Ikiwa mtu aliyepewa wito uliotajwa katika kifungu cha 15 cha Sheria hii hakuhudhuria mbele ya Baraza au Kamati, Spika anaweza, baada ya kuridhika kuwa wito huo umefikishwa au mtu aliyepewa wito kwa makusudi ameepuka kupokea wito huo, atatoa hati ya kumkamata na kumleta kwa wakati na mahali palipotajwa katika hati, mbele ya Baraza au Kamati. |

(2) Hati iliyotolewa chini ya kifungu hiki itatekelezwa na Afisa wa Polisi.

(3) Spika anaweza, kuhusiana na kutoa hati ya kukamatwa chini ya kifungu hiki, ikiwa anaona inafaa, baada ya kuidhinisha katika hati hiyo, kuamuru mtu huyo aliyetajwa katika hati hiyo aachiliwe baada ya kukamatwa kwa ajili ya kuhudhuria katika Baraza au Kamati kama inavyohitajika kuidhinishwa.

(4) Hati ya kukamata iliyotolewa chini ya masharti ya kifungu hiki, itakuwa kama ilivyoelezwa katika Jadweli la Tatu la Sheria hii.

Shahidi anaweza kuhojiwa kwa kiapo.

**17.**-(1) Baraza au Kamati iliyoidhinishwa inaweza kuhitaji maelezo yoyote, jambo na kitu kinachohusiana na suala linalochunguzwa mbele ya Baraza au Kamati kuthibitishwa au vyenginevyo kusahihishwa kwa njia ya mdomo wa shahidi na anaweza kupelekea mashahidi hao kuhojiwa kwa njia ya kiapo.

(2) Kiapo kinachohitajika kuchukuliwa chini ya masharti ya kifungu hiki, kinaweza kusimamiwa na Katibu au mtu mwengine yeyote aliyeteuliwa na Spika kwa ajili ya kazi hiyo au ikiwa ni shahidi mbele ya Kamati, Mwenyekiti au Katibu wa Kamati.

Kukataa kujibu suali au kutoa nyaraka.

**18.**-(1) Endapo mtu yeyote aliyeamriwa kuhudhuria au kutoa ushahidi au kuwasilisha nyaraka yoyote mbele ya Baraza au Kamati, anakataa kujibu suali lolote ambalo anaulizwa au kuwasilisha nyaraka yoyote kwa madai kuwa ni jambo la kibinafsi na haitoathiri jambo linalofanyiwa uchunguzi, Spika au Mwenyekiti wa Kamati baada ya kuridhika na sababu zilizotolewa, anaweza kumruhusu asijibu au kuwasilisha jambo hilo.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mtu yeyote anayekataa kuhojiwa au kujibu maswali halali na muhimu yanayoulizwa au kuwasilisha nyaraka na Baraza au Kamati isipokuwa kwamba kukataa huko kumesamehewa kama ilivyoelezwa kabla, atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atalipa faini isiyozidi Shilingi za Kitanzania Milioni Moja au kifungo kisichozidi mwaka mmoja au vyote viwili faini na kifungo.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Baraza au Kamati litakuwa na uwezo wa kujiwekea taratibu zake zinazohusiana na njia na taratibu za kuchukulia ushahidi.

Fursa za shahidi.

**19.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya vifungu vidogo vya (2) na (3) vya kifungu hiki, mtu aliyeitwa kutoa ushahidi, kufichuwa mawasiliano au kuwasilisha nyaraka yoyote mbele ya Baraza au Kamati atakuwa na haki na fursa sawa kama atakavyotoa mbele ya Mahakama.

(2) Isipokuwa kama Rais ataelekeza vyenginevyo kwa maandishi, Afisa wa Umma hatokataa:

(a) kutoa ushahidi mbele ya Baraza au Kamati;

(b) kuwasilisha nyaraka yoyote mbele ya Baraza au Kamati; au

(c) kuwasilisha katika Sekretarieti taarifa yoyote inayohusiana na mawasiliano ya idara yoyote ya Serikali au jambo lolote linaloathiri huduma za utumishi wa umma.

(3) Jibu la mtu aliyeulizwa suali katika Baraza au Kamati halitakuwa ushahidi utakaokubalika dhidi yake katika taratibu za jinai au madai isipokuwa katika taratibu za jinai chini ya makosa ya ushahidi wa uongo, kula njama ya kutoa ushahidi wa uongo, kutunga ushahidi, kudanganya mashahidi na kuharibu ushahidi chini ya Sheria ya Adhabu au kosa dhidi ya Sheria hii.

Ushahidi wa Mwenendo wa Mashauri katika Baraza au Kamati kutokuto-lewa bila ya ruhusa.

**20.**-(1) Bila ya kujali masharti ya sheria nyengine yoyote, Mjumbe au Afisa wa Baraza na mtu aliyeombwa kuchukuwa kumbukumbu za ushahidi mbele ya Baraza au Kamati yoyote isipokuwa kama ilivyoelezwa katika Sheria hii, hatotoa ushahidi popote kuhusiana na maudhui ya nyaraka yoyote iliyowasilishwa mbele ya Baraza au Kamati hiyo kama vile itakavyokuwa au kuhusiana na shauri lolote au mahojiano yaliyofanywa mbele ya Baraza au Kamati vyovyote vile itakavyokuwa bila ya kupata ruhusa maalum ya Baraza.

(2) Ruhusa maalumu iliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, inaweza kutolewa na Spika wakati wa mapumziko au kuakhirishwa kwa Baraza, au ikiwa hayupo au dharura nyengine au wakati wa kuvunjwa kwa Baraza inaweza kutolewa na Katibu.

Cheti kwa Shahidi.

**21.**-(1) Shahidi aliyeitwa mbele ya Baraza au Kamati ambaye amejibu kwa kikamilifu na uaminifu suali lolote aliloulizwa na Baraza au Kamati na ikiridhika, anaweza kupewa cheti kinachoeleza kwamba shahidi huyo amehojiwa na amejibu maswali yote kama ilivyotakiwa.

(2) Cheti kilichotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ikiwa ni shahidi aliyeitwa mbele ya Baraza kitatiwa saini na Spika, na ikiwa ni shahidi aliyeitwa mbele ya Kamati kitatiwa saini na Mwenyekiti wa Kamati.

(3) Spika, baada ya kushauriana na Mkurugenzi wa Mashtaka, ikiwa ataridhika kwamba:

(a) cheti kilichotolewa kwa shahidi baada ya kutoa taarifa za uongo; au

(b) ushahidi uliotolewa na shahidi umehesabiwa kuwa wa kupotosha Baraza au Kamati yoyote,

atafuta cheti na shahidi huyo atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani ataadhibiwa kama vile ametenda kosa la udanganyifu chini ya Sheria ya Adhabu.

(4) Shahidi ambaye amepewa cheti chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, anaweza kukitumia cheti hicho Mahkamani kama ushahidi na Mahkama inaweza kumzingatia kuwa shahidi huyo ni mkweli.

(5) Endapo cheti kimefutwa chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, shahidi ambaye alipewa cheti atakuwa hastahiki ulinzi wowote uliotolewa chini ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki.

(6) Cheti kilichotolewa katika kifungu hiki kitakuwa kama kilivyoainishwa katika Jadweli la Nne la Sheria hii.

Ushahidi wa uongo.

**22.** Mtu ambaye mbele ya Baraza au Kamati kwa makusudi ametoa jibu la uongo kwa suali lolote aliloulizwa wakati wa mahojiano yoyote, atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa hatiani, ataadhibiwa kama kwamba ametenda kosa la udanganyifu lililoelezwa chini ya Sheria ya Adhabu.

Kuingilia ushahidi.

**23.** Mtu ambaye:

(a) anaharibu, anazuia, anatishia, anashawishi au kwa njia yoyote ile anatumia vibaya uhusiano wake kwa shahidi yeyote juu ya ushahidi ambao anautoa mbele ya Baraza au Kamati; au

(b) anatishia, anashawishi au kwa njia yoyote anaadhibu, analaumu au anajeruhi au kujaribu kuadhibu, kulaumu au kujeruhi mtu yeyote kwa kuwa ametoa ushahidi mbele ya Baraza au Kamati,

atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Laki Tatu au kifungo kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote viwili, faini na kifungo.

Waraka wa uongo.

**24.** Mtu ambaye atawasilisha katika Baraza au Kamati waraka wowote wa uongo, usiyokuwa wa kweli, uliyotungwa au uliyoghushiwa kwa nia ya kulipotosha Baraza au Kamati, kama kitendo hicho hakijaelezwa kuwa ni kosa chini ya kifungu cha 19 cha Sheria hii, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atahukumiwa kama vile ametenda kosa la kughushi chini ya Sheria ya Adhabu.

Kudharau.

**25.** Mtu ambaye:

(a) baada ya kuitwa kutoa ushahidi mbele ya Baraza au Kamati anakataa kuapishwa au kutoa uthibitisho bila ya sababu za msingi;

(b) ni shahidi mwenye kukosa nidhamu;

(c) anasababisha kizuizi au usumbufu ndani ya maeneo ya Baraza wakati Baraza au Kamati inaendelea;

(d) anaonesha uvunjifu wa heshima kwa maneno au vitendo dhidi ya Spika au Mwenyekiti wa Kamati; au

(e) anafanya kitendo chengine chochote cha kuvunja heshima kwa makusudi au kuhusiana na mwenendo wa Baraza au Kamati au kwa mtu yeyote anayeendesha shughuli hizo,

atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Laki Tatu au kifungo kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote viwili, faini na kifungo.

Maswali yanayohusiana na maamuzi ya ushahidi na utoaji wa nyaraka.

**26.** Ikiwa katika muda wowote suali lolote linatokea katika Baraza au Kamati kuhusu:

(a) haki au uwezo wa Baraza au Kamati kusikiliza, kukubali au kupokea ushahidi wa mdomo;

(b) haki au uwezo wa Baraza au Kamati kusoma au kuchunguza waraka wowote, kitabu, kumbukumbu au nyaraka au kumwita, kuelekeza au kumwita mtu yeyote awasilishe waraka wowote, kitabu, kumbukumbu au nyaraka mbele ya Baraza au Kamati; au

(c) haki au fursa ya mtu yeyote ikijumuisha Mjumbe wa Baraza au Kamati,

kwamba suala hilo litakuwa, kwa kuzingatia mwenendo wa masharti ya Sheria hii na isipokuwa kama imeelezwa katika masharti haya ya kuamua maswali, yataamuliwa kwa kuzingatia utamaduni wa vyombo vya kutunga sheria.

Taratibu za Baraza kuwa za kimahakama.

**27.** Utaratibu wowote wa Baraza au Kamati ambao mtu yeyote hutoa ushahidi au huwasilisha nyaraka, utahesabika kama ni utaratibu wa kimahkama kwa madhumuni ya makosa yanayohusiana na kutoa ushahidi wa uongo, kula njama, kutunga ushahidi, kudanganya mashahidi na kuharibu ushahidi chini ya Sheria ya Adhabu.

## SEHEMU YA NNE
## MAKOSA NA ADHABU

Kosa kuhusu uingiaji katika Baraza.

**28.** Mtu ambaye:

(a) ni mgeni anaingia au kujaribu kuingia katika eneo la Baraza kwa kujua, kinyume na amri yoyote iliyotolewa na Spika;

(b) ni mgeni anashindwa au anakataa kuondoka katika eneo la Baraza ambapo amri ya kuondoka imeshatolewa na Spika au Afisa wa Baraza;

(c) ni mgeni, anakiuka amri yoyote iliyowekwa na Spika chini ya Sheria hii inayohusiana na ruhusa ya uingiaji wa wageni katika eneo la Baraza au kanuni yoyote iliyotolewa na Spika chini ya maagizo ya Kanuni za Kudumu; au

(d) anahudhuria kikao chochote cha Baraza kama mwakilishi wa chombo chochote cha habari baada ya kupewa ruhusa chini ya amri yoyote iliyotolewa chini ya Sheria hii au Kanuni za Kudumu kuwa mwakilishi wa Chombo hicho cha Habari ameondolewa,

atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Laki Mbili lakini isiyozidi Laki sita au kifungo kisichopungua mwezi mmoja lakini kisichozidi miezi mitatu au vyote viwili, faini na kifungo.

Rushwa au utendaji mbaya.

**29.-**(1) Mtu ambaye anampa Mjumbe au Afisa wa Baraza au mtumishi wa umma yeyote au Mshirika wa Mjumbe au Afisa wa Baraza ama moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja, rushwa, zawadi au tunzo yoyote kwa lengo la kumshawishi Mjumbe huyo au Afisa wa Baraza au mtumishi wa umma yeyote au Mshirika wa Mjumbe katika kazi zao kwa lengo la kumshawishi Mjumbe au Afisa kukubali au kuupinga mswada wowote au azimio au jambo lililowasilishwa au lililokusudiwa kuwasilishwa katika Baraza, atakuwa ni mkosa.

(2) Mjumbe au Afisa wa Baraza au mtumishi wa umma yeyote au Mshirika wa Mjumbe au Afisa wa Baraza anayeomba, anayepokea, anayekubali, moja kwa moja au vyenginevyo, rushwa yoyote, zawadi au tunzo inayotolewa ambayo itakuwa ni kosa chini ya kifungu hiki, atakuwa ni mkosa.

(3) Mtu ambaye anafanya kosa chini ya kifungu hiki na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Tatu au atatumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano au vyote viwili, faini na kifungo.

(4) Wakati kosa litakapothibitika dhidi ya mtu yeyote chini ya kifungu hiki, Mahkama inaweza kutoa agizo kwamba thamani au kiwango chochote cha rushwa au zawadi kilichotolewa kitaifishwe au kirejeshwe au kifidiwe kwa namna ile ile iliyoelezwa chini ya Sheria ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi ya Zanzibar au sheria nyengine yoyote.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, neno "mshirika" linajumuisha mume au mke, au msaidizi wa Mjumbe au Afisa wa Baraza na mtu mwengine yeyote ambaye yupo karibu na Mjumbe au Afisa wa Baraza.

Makosa mengine dhidi ya Mjumbe na Afisa wa Baraza.

**30.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anamshambulia, anamzuia au anamtukana Mjumbe yeyote au Afisa wa Baraza anayekwenda au anayetoka katika maeneo ya Baraza, au sehemu yoyote ambayo Kamati inakutana;

(b) anajaribu kumshurutisha ama moja kwa moja au kwa namna isiyo ya moja kwa moja, Mjumbe yeyote kwa nguvu, matusi au vitisho kujitangaza kupendelea au kupinga mswada wowote, azimio, jambo, uamuzi au mambo yaliyowasilishwa au yanayokusudiwa kuwasilishwa kwenye Baraza;

(c) anamshambulia, anaingilia, anapinga au anamzuia Afisa yeyote wa Baraza wakati akitekeleza wajibu wake;

(d) anatuma kwa Mjumbe au Afisa yeyote wa Baraza barua yoyote ya kitisho, ujumbe ukiwemo kutoka katika mitandao ya kijamii au kutaka kupigana naye juu ya kitendo alichokifanya kama Mjumbe au Afisa wa Baraza; au

(e) anamshambulia au anamzuia Mjumbe yoyote wakati anatekeleza shughuli za uwakilishi Jimboni.

atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Moja au kifungo kisichopungua miaka mitatu au vyote viwili, faini na kifungo.

Kukosa utiifu.

**31.**-(1) Mtu ambaye kwa makusudi na bila ya kuzuiliwa na sheria anashindwa kufuata au anakwenda kinyume na amri yoyote iliyotolewa chini ya kifungu cha 11 au

16 vya Sheria hii, amesababisha au ameshiriki katika fujo lolote ambalo linaingilia au linaelekea kuingilia mwenendo wa Baraza au Kamati yoyote wakati Baraza au Kamati imekaa au kwa makusudi ameshindwa kutii amri nyengine yoyote ya Baraza na kuleta usumbufu katika utekelezaji wa kazi zake, atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atalipa faini isiyozidi Shilingi za Kitanzania Laki Tano au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote viwili, faini na kifungo.

(2) Hakuna kosa litakalofanywa chini ya kifungu hiki isipokuwa Spika au Afisa wa Baraza amemjuulisha mtu anayehusika kwamba kushindwa au kutotii huko ni kwenda kinyume na amri hiyo aliyopewa na mtu huyo akaendelea kutotii au kwenda kinyume kama ilivyoelezwa.

Makosa mengine.

**32.**-(1) Mtu ambaye:

(a) anaeneza taarifa za uongo au kashfa kwa Baraza au Kamati yoyote ambazo kwa makusudi zinapotosha kwa hali yoyote mwenendo wa Baraza au Kamati;

(b) anaeneza isipokuwa kwa ruhusa ya jumla au makhsusi ya Baraza taarifa yoyote ya shughuli za mkutano wa Baraza au Kamati wakati shughuli hizo hazikutangazwa kwa umma;

(c) anaeneza isipokuwa kwa ruhusa ya jumla au makhsusi ya Baraza, waraka wowote, taarifa au waraka mwengine ulioandaliwa kwa ajili ya kuwasilishwa katika Baraza kabla ya taarifa hiyo kuwasilishwa Mezani;

(d) anatoa au kusababisha kutoa nakala ya sheria yoyote inayofanyakazi au nakala ya taarifa yoyote, waraka, makala ya Baraza kama inavyokusudiwa kuchapishwa na Mpiga chapa wa Serikali au chini ya mamlaka ya Baraza au Spika na taarifa hiyo haikuchapishwa;

(e) anatoa katika ushahidi nakala yoyote hiyo kama inavyokusudiwa kuchapishwa kwa kujua kwamba taarifa hiyo haikuchapishwa; au

(f) anaeneza au anachapisha kashfa yoyote kwa Mjumbe yeyote kuhusiana na tabia au mwenendo wake kama ni Mjumbe au kwa kuzingatia kitendo alichokifanya au maneno aliyoyatoa katika kipindi cha kutekeleza shughuli za Baraza,

atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Moja au kifungo kisichozidi miaka mitatu au vyote viwili, faini na kifungo.

(2) Mtu ambaye anatumia bendera ya Baraza kinyume na kifungu cha 8 cha Sheria hii, au Kanuni zilizotungwa kuhusiana na matumizi ya bendera hiyo, ametenda kosa na atakapotiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Moja au kifungo kisichozidi miaka mitatu au vyote viwili, faini na kifungo.

Kupokea rushwa kwa Mjumbe.

**33.** Mjumbe yeyote ambaye anatoa, anapokea, anakubali, anapata, anajaribu kutoa au kupokea rushwa, tunzo, takrima, zawadi au faida ya aina yoyote kwa ajili yake au mtu mwengine yeyote kwa lengo la kusema, kupiga kura au kuigiza kuwa ndiye aliyesema, aliyepigiwa kura au kuigiza au anaacha kuigiza, ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Tatu au kifungo kisichozidi miaka mitano au vyote viwili, faini na kifungo.

Kulindwa kwa mtu anayechapisha kwa mamlaka ya Baraza.

**34.**-(1) Mtu au mtumishi wake ambaye kosa la madai au jinai limefunguliwa dhidi yake kwa kusambaza taarifa yoyote, waraka, kumbukumbu za kikao, uamuzi wa kura na mwenendo wa kikao anaweza, baada ya kutoa indhari ya maandishi ya saa arobaini na nane mahakamani, kuwasilisha cheti kilichosainiwa na Spika, kitakachothibitisha kuwa usambazaji huo alioufanya yeye au mtumishi wake, ulifanyika kwa amri ya agizo la Baraza.

(2) Mahkama, baada ya kupokea cheti hicho pamoja na hati ya kiapo, itakihakiki na Mahkama hiyo wakati huo huo itayafuta mashtaka hayo ya madai au jinai na hatua inayoendelea na iliyopangwa kuendelea itachukuliwa kuwa imeshamalizika

Kutangaza mwenendo wa kesi bila ya nia ovu.

**35.** Katika kesi yoyote ya madai iliyofunguliwa kwa kutangaza ripoti yoyote au muhtasari wake au dondoo yoyote au ufupisho wa ripoti, waraka, kumbukumbu za kikao, kura na majadiliano ya ndani ya Baraza, ikiwa Mahkama itaridhika kwamba ripoti, muhtasari, dondoo, ufupisho wa ripoti hiyo imetangazwa kwa nia njema na sio kwa nia ovu, hukumu itatolewa kwa upande wa mlalamikiwa.

Mtu asiyekuwa na sifa kukaa au kupiga kura ndani ya Baraza.

**36.** Mtu ambaye:

(a) amechaguliwa au ameteuliwa kuwa Mjumbe wa Baraza lakini hajatimiza masharti ya kumuwezesha kukaa au kupiga kura ndani ya Baraza; au

(b) amekaa au kupiga kura ndani ya Baraza baada ya kiti chake kuwa wazi au amekosa sifa ya kukaa au kupiga kura, kwa kujua au kuwa na sababu za msingi za kuamini kwamba hakutimiza masharti muhimu yanayohitajika kukaa au kupiga kura au kiti chake kimekuwa wazi kwa namna itakayokuwa;

atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Laki Mbili na Hamsini Elfu kwa kila siku ambayo amekaa na kupiga kura.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA JUMLA

Kutokamatwa bila ya idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

**37.** Hakuna Mjumbe atakayekamatwa au kuwekwa kizuizini kwa tuhuma ya kutenda kosa la jinai lililofanywa wakati wa kutekeleza majukumu yake, isipokuwa kwa idhini iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mashtaka.

Taarifa juu ya kukamatwa kwa Mjumbe.

**38.**-(1) Endapo Mjumbe akikamatwa kwa shitaka la jinai au akihukumiwa kifungo na Mahkama, mamlaka husika itaeleza mara moja taarifa hiyo kwa Spika ikionesha sababu za kukamatwa, kuwekwa kizuizini au kufungwa kama itakavyokuwa na mahali atakapowekwa kizuizini au kufungwa Mjumbe huyo.

(2) Endapo Mjumbe amekamatwa na baada ya kutiwa hatiani, kuachiwa kwa dhamana akisubiri rufaa au kuachiwa vyenginevyo, Spika atapewa taarifa hiyo na mamlaka inayohusika.

(3) Itakuwa ni haki ya Baraza kupokea taarifa mara moja kutoka kwa Spika juu ya kukamatwa, kuwekwa kizuizini, kutiwa hatiani, kufungwa na kuachiliwa kwa Mjumbe.

Kinga.

**39.** Spika, Mjumbe, Afisa wa Baraza au mtu mwengine yeyote hatokuwa na dhima kwa jambo lolote alilolifanya kwa nia njema wakati anatumia uwezo wowote, anatekeleza jukumu lolote au anafanya kazi yoyote kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, Kanuni au Amri iliyotolewa chini ya masharti ya Sheria hii.

Uwezo wa Mpambe wa Baraza.

**40.** Kila Mpambe wa Baraza, kwa madhumuni ya Sheria hii na katika utekelezaji wa masharti ya Sheria ya Jinai ndani ya eneo la Baraza, atakuwa na mamlaka yote na fursa zote za Afisa wa Polisi.

Uwezo wa kukamata.

**41.** Mpambe wa Baraza anaweza kukamata bila ya kuwa na hati ya ukamataji:

(a) mtu ambaye anatenda kosa lolote mbele yake, kinyume na kifungu cha 30 au 31 cha Sheria hii; au

(b) mtu ambaye katika hali ya kawaida atamshuku kuwa ametenda kosa au anataka kutenda kosa kinyume na kifungu chochote kilichotajwa katika Sheria hii.

Idhini kwa ajili ya mashtaka.

**42.**-(1) Hakuna mashtaka dhidi ya kosa chini ya Sheria hii litakalofunguliwa isipokuwa kwa idhini ya maandishi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, Mkurugenzi wa Mashtaka maana yake ni Mkurugenzi wa Mashtaka, Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka au Kaimu Mkurugenzi wa Mashtaka.

Taarifa Rasmi iliyochapishwa kutokana na amri ya Baraza kukubaliwa kwa ajili ya ushahidi.

**43.** Wakati wa uchunguzi wowote unaohusiana na fursa, kinga na uwezo kwa Baraza au Mjumbe yeyote, nakala yoyote ya Taarifa Rasmi au Kanuni za Kudumu zilizochapishwa au zilizothibitishwa na kutiwa saini na Katibu, zitakubaliwa kama ushahidi katika mahkama na mahali popote bila ya uthibitisho mwengine wowote kutolewa.

Hadhi ya uwezo chini ya Sheria hii.

**44.** Uwezo wa Baraza na Spika uliotolewa chini ya Sheria hii, utakwenda sambamba na uwezo uliotolewa na Katiba au Kanuni za Kudumu.

Kutokuwepo kwa Spika au Naibu Spika.

**45.-**(1) Kwa madhumuni ya kifungu hiki "kutokuwepo" kuhusiana na Spika au Naibu Spika, maana yake:

(a) Ofisi ya Spika au ofisi ya Naibu Spika iko wazi; au

(b) Spika au Naibu Spika hana uwezo au anazuiliwa kutokana na sababu yoyote kutekeleza majukumu ya Baraza.

(2) Katika kipindi chochote ambacho Spika hatokuwepo, uwezo na fursa aliyopewa Spika na Sheria hii, atapewa Naibu Spika kwa kuzingatia masharti ya Katiba.

(3) Kwa kipindi chochote ambacho wote Spika na Naibu Spika watakuwa hawapo:

(a) uwezo na fursa aliyopewa Spika katika masharti ya vifungu vyengine isipokuwa vifungu vya 21 na 34 vya Sheria hii, utakuwa:

(i) unaohusiana na jambo lolote linalotokana na kikao cha Baraza katika utekelezaji wa shughuli utatolewa kwa Mjumbe wa Baraza kama atakavyochaguliwa na Baraza kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 81 cha Katiba kuongoza kikao cha Baraza wakati mambo kama hayo yanatokea; na

(ii) unaohusiana na jambo jengine lolote ambalo atapewa Mjumbe;

(b) uwezo aliyopewa Spika katika kifungu cha 21 na 34 cha Sheria hii, atapewa Katibu.

Tuhuma juu ya afya ya akili ya Mjumbe.

**46.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Kudumu, endapo Mjumbe atatuhumiwa kuwa hana akili timamu au anaugua ugonjwa wa akili, Spika atateua jopo la watu watatu ambao sio wajumbe wa Baraza kuchunguza tuhuma hiyo na kuwasilisha ripoti yao kwa Spika.

(2) Jopo lililoteuliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki litawajumuisha:

(a) Jaji wa Mahkama Kuu ya Zanzibar kama Mwenyekiti;

(b) Madaktari wawili ambao wamebobea katika fani ya magonjwa ya akili watakaoteuliwa na Bodi ya Madaktari.

(3) Spika, baada ya kupokea ripoti na kupatikana majibu kutoka katika jopo, ataiwasilisha ripoti hiyo katika Baraza kwa ajili ya uamuzi wa mwisho.

Katibu kuandaa toleo juu ya Haki na Fursa za Mjumbe.

**47.** Katibu, baada ya kuamriwa kuandaa matoleo na Kamati ya Uongozi ya Baraza atatoa matoleo akielezea na kufafanua stahiki, haki na fursa za Viongozi, Wajumbe na Maafisa wa Baraza.

Wajibu wa Mjumbe.

**48.** Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 88 cha Katiba, Mjumbe atakuwa na wajibu ufuatao:

(a) kulinda heshima ya Baraza na Kamati zake na asijihusishe na vitendo viovu vitakavyopelekea Baraza au Kamati zake kudharauliwa; na

(b) kutumia vikao vya Baraza na Kamati katika kutetea haki na maslahi ya raia kwa mujibu wa masharti ya Katiba, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 na maadili ya kitaifa.

Yasiyohusika kwa Wajumbe na Maafisa wa Baraza.

**49.**-(1) Mjumbe hatokuwa Mjumbe wa Bodi ya Shirika au Taasisi yoyote ya Umma isiyokuwa ya Baraza.

(2) Mjumbe au Afisa wa Baraza hatokuwa mshauri wa Mahkama yoyote au Baraza lolote la uamuzi.

(3) Mjumbe au Afisa wa Baraza wakati anahudhuria kikao cha Baraza au Kamati, hatotakiwa kufika kama shahidi mbele ya Mahkama yoyote, Baraza la uamuzi au Tume ya Uchunguzi au mamlaka nyengine yoyote inayofanana.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, utoaji wa hati iliyosainiwa na Spika au Mwenyekiti wa Kamati utachukuliwa kuwa ni ushahidi wa kutosha kwa Mjumbe au Afisa wa Baraza kuwa anahudhuria kikao cha Baraza au Kamati.

Adhabu kwa Mjumbe.

**50.**-(1) Mjumbe ambaye anayekiuka masharti ya kifungu cha 49 cha Sheria hii, anaweza kusimamishwa na Baraza kushiriki katika shughuli za Baraza na Kamati zake.

(2) Ikiwa Mjumbe amesimamishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kusimamishwa kwake kutakuwa:

(a) kwa kosa la kwanza ni siku ishirini na moja;

(b) kwa kosa la pili hadi siku sitini; na

(c) katika kosa la tatu au zaidi, mpaka Baraza litakapoamua kusitisha kusimamishwa kwa Mjumbe huyo.

(3) Mjumbe ambaye amesimamishwa katika Baraza ataondoka mwenyewe kutoka katika maeneo ya Baraza na hatastahiki kulipwa posho yoyote isipokuwa mshahara, posho la uwakilishi na nyumba kwa kipindi chote cha kusimamishwa.

(4) Utaratibu wa kumsimamisha Mjumbe chini ya kifungu hiki, utakuwa kama ulivyoelezwa katika Kanuni za Kudumu.

Adhabu ya jumla.

**51.** Endapo mtu atakiuka masharti ya kifungu chochote cha Sheria hii, kanuni au amri yoyote iliyowekwa chini ya Sheria hii ambapo adhabu yake haikutajwa, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyozidi Shilingi Laki Tano za Kitanzania au kifungo kisichozidi miezi sita au vyote viwili, faini na kifungo.

Kutotekelezwa kwa Hukumu.

**52.** Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 71(3) cha Katiba na masharti ya vifungu vyengine vya Katiba vinavyohusika, hakuna uamuzi au amri itakayotekelezwa dhidi ya Mjumbe yeyote ambaye ametenda kosa lolote la madai au jinai kabla ya kumalizika kwa muda ulioruhusiwa kukata rufaa au ambapo hakuna muda uliotolewa kukata rufaa, hakuna utekelezaji utakaofanywa kabla ya kumalizika kwa muda wa miezi miwili tangu siku ambayo hukumu au amri ilipotolewa.

Kanuni.

**53.** Waziri kwa kushauriana na Spika, anaweza kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

Kufuta na kubakiza.

**54.**-(1) Sheria ya Baraza la Wawakilishi (Kinga, Uwezo na Fursa), Nam. 4 ya 2007 inafutwa.

(2) Bila ya kujali ufutaji chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, jambo lolote lililofanywa chini ya Sheria iliyofutwa, litachukuliwa kuwa limetekelezwa chini ya masharti ya Sheria hii.


**JADWELI LA KWANZA**

**[Chini ya kifungu cha 8(1)]**

---

**BENDERA YA BARAZA**

Ina rangi ya buluu bahari, umbo la mstatili na nembo ya Afisi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar kati kati.



**JADWELI LA PILI**

**[Chini ya kifungu cha 15(4)]**

---

# HATI YA WITO

**KWENDA KWA** Bw./Bi. ..........................................................................................................................

**KWAMBA BARAZA/KAMATI** ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar inakutaka ufike mbele ya BARAZA/KAMATI siku ya ............................................., 20............., saa .................. kamili katika eneo la ............................, kuhusiana na jambo/shauri linalohusiana na ........................ ............................................................................................................................................................ ............................................. kwa ajili ya kutoa ushahidi.

Zingatia kwamba, kushindwa kwako kuhudhuria katika siku hiyo katika wakati na mahali palipotajwa, Baraza/ Kamati itaendelea na shughuli zake na kuamua kuwa umekataa kuhudhuria. Imetolewa na kutiwa saini na Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar

............................

***SAINI***

**MUHURI**

**JADWELI LA TATU**

**[Chini ya kifungu cha 16(4)]**

---

# HATI YA KUKAMATA

**KWENDA KWA:**

Askari Polisi

**KWA KUWA** Bw./Bi. ....................................................... amepewa Hati ya Wito ipasavyo lakini ameshindwa kuhudhuria (ametoroka au kujiepusha kupewa wito). Unaamrishwa kumkamata na kumfikisha **BWANA/BIBI** .......................................... mbele ya Baraza/Kamati.

Unaamriwa zaidi kurudisha Hati hii siku au kabla ya .................... siku ya ....................20..... saa .............. katika eneo la ....................na idhini inayothibitisha siku na namna ambayo imetekelezwa au sababu kwa nini haijatekelezwa.

Imetolewa na kutiwa saini na Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar

............................

***SAINI***

**MUHURI**

**JADWELI LA NNE**

**[Chini ya kifungu cha 21(6)]**

---

# CHETI CHA SHAHIDI

Inathibitishwa hapa kwamba Bw./Bi. ……………………………………………………………… ambaye amepewa hati ya wito wa kuwa shahidi mbele ya Baraza/Kamati ya Baraza la Wawakilishi, amehojiwa kwa ukamilifu na kwa uaminifu amejibu maswali aliyoulizwa kwa namna ambayo Baraza/Kamati imeridhika.

Imetolewa na kutiwa saini na Spika/Mwenyekiti wa Kamati/Katibu.

…………………………..…

***SAINI***

**MUHURI**

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 7 Septemba, 2022.

……………………………………………

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***